

JINA LA MRADI: Mradi wa Kuhamasisha Mbinu Bora na Rafiki kwa Mazingira za kupunguza uzalishwaji wa Kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu zitokanazo na uchomaji wa taka katika nchi za SADC (Open Burning)

MFADHILI WA MRADI: GEF kupitia UNIDO

LENGO LA MRADI: Kuendelea kupunguza uchomaji wa taka unaosababisha kuzalishwa kwa kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu katika nchi za SADC zinazotekeleza mradi

MUDA WA UTEKELEZAJI: 2018 - 2021

BAJETI YA MRADI: USD 96,800

ENEO LA UTEKELEZAJI: Manispaa za Kigamboni na Ubungo

SHUGHULI ZA MRADI

1. Kuainisha wataalam wawili watakaoshiriki kuandaa nyaraka za hali ya uzalishwaji wa kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu.
2. Kutembelea madampo na kukusanya taarifa za hali ya uchomaji taka katika maeneo hayo.
3. Kuainisha Taasisi ya Serikali itakayofanya semina mbili za kuhamasisha mbinu bora na rafiki kwa mazingira za kupunguza uchomaji wa taka.
4. Kuimarisha uwezo wa nchi wa kudhibiti uchomaji taka wa wazi kupitia mafunzo kwa watumishi wa umma na wadau wengine muhimu kwa kutumia mbinu bora za kimazingira.
5. Kuanzisha mchakato wa kuandaa au kupitia Sera na Sheria zilizopo ili kuona kama zimegusa masuala ya kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu.
6. Kufanya kikao cha wadau wakiwemo Sekta binafsi zinazojihusisha na usimamizi wa taka ili kuainisha fursa za kibiashara.
7. Kuunda Kamati ndogo ya usimamizi wa mradi kwa kushirikiana na mratibu
8. Kufanya tathmini na ufuatiliaji wa mradi.
9. Kushiriki katika vikao vya Kamati elekezi ya mradi.
10. Kutambua fursa zilizopo katika urejelezaji wa taka ili kuanzisha mradi wa mfano katika mfumo wa utenganishaji na ukusanyaji wa taka.
11. Kuzisaidia Manispaa za Kigamboni na Ubungo kuandaa Mipango ya usimizi wa taka kwa kutumia mbinu rafiki kwa mazingira.
12. Kuwezesha uanzishwaji wa kaznidata ya uchomaji wa taka usio salama na kutoa mafunzo ya namna ya kuiendeleza kaznidata husika.